

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
FOMU YA KUJIUNGA NA ELIMU YA SEKONDARI KIDATO CHA KWANZA 2021
MTUA SEKONDARI.

MZAZI/MLEZI WA

.....

UTANGULIZI

Natumia fursa hii kumpongeza mwanao kwa kuchaguliwa kuendelea na elimu ya Sekondari kidato cha kwanza mwaka **2021** tunamkaribisha sana.

Anatakiwa kuripoti Shuleni bila kukosa tarehe **11/01/2021** Saa **1:00** asubuhi.endapo atachelewa kuripoti hadi tarehe **19/01/2021** mzazi utachukuliwa hatua za kisheria

MAHITAJI YA MWANAFUNZI

1. A SARE ZA SHULE

(i) MAVAZI YA DARASANI (wavulana)

- Suruali nyeusi mbili **(2)** za heshima (zisiwe za kubana -modo)
- Mashati mawili **(2)** meupe mikono mifupi
- Mikanda miwili **(2)** ya ngozi rangi nyeusi
- Viatu vya ngozi vyenye Kamba nyeusi
- Soksi nyeupe jozi mbili **(2)**
- Fulana rangi ya kijivu yenye Nembo ya shule

(ii) MAVAZI YA DARASANI (WASICHANA)

- Sketi nyeusi mbili **(2)** za heshima kitambaa kizito
- Mashati mawili **(2)** meupe mikono mifupi
- Hijabu inaruhusiwa iwe nyeupe nusu kanzu mikono mirefu.
- Viatu vyeusi vya ngozi kisigino kifupi (**Bajaji haziruhusiwi**)
- Soksi nyeupe jozi mbili **(2)**
- Fulana rangi ya kijani yenye Nembo ya shule (**Form six**)

(iii) MAVAZI YA MICHEZO KWA WOTE

- Raba rangi yoyote
- Fulana ya bluu au njano **(jezi)**
- Bukta ya njano/kijani (wavulana)
- Traki suti ya njano/bluu wasichana.

B. MAHITAJI YA KITAALUMA

- Daftari kumi (**counter books**)
- kalamu za wino na Risasi (**peni & pencils**)
- Mkebe
- Kamusi (**dictionary**)
- Karatasi Bunda 1 (**ream**)

2. KANUNI NA TARATIBU ZA SHULE

Shule hii inaendeshwa kwa mujibu wa sharia ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na inazingatia miongozo yote inayotolewa na wizara zenye dhamana ya Elimu nchini. Mwanafunzi anatakiwa kuzingatia taratibu mbalimbali zilizowekwa.

A. SHERIA NA KANUNI ZA SHULE

- (i) Mwanafunzi awe na heshima na adabu kuanzia nyumbani, shulenii na Mtaani.
- (ii) Mwanafunzi haruhusiwi kutumia lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu na watu wengine wote
- (iii) Awe na moyo wa kushirikiana, huruma, upole na kusaidiana katika shughuli mbalimbali pamoja na kazi.
- (iv) Mwanafunzi atasimama kusalimia na kupokea mzigo wa mwalimu au mtu yejote anayemzidi umri.
- (v) Mwanafunzi haruhusiwi kwenda kwenye nyumba za walimu bila kuruhusiwa na mwalimu au mkuu wa shule.
- (vi) Mwanafunzi haruhusiwi kufanya yafuatayo
 - (a) Kuvuta sigara/Bangi
 - (b) Kutumia aina yoyote ya madawa ya kulevyia
 - (c) Kuvalaa mavazi yasiyo ya heshima mfano kulegeza suruali, kuvalaa nguo zaa kubana n.k
 - (d) Kupiga kelele darasani.
 - (e) Kufuga kucha ndefu, nywele ndefu na kuvalaa mapambo, kujipaka rangi ya kucha na midomo (kwa wasichana).
 - (f) Kunyoa nywele kwa mitindo au kipara (viduku)
 - (g) Kuchelewa kwa makusudi shulenii, kutofanya kazi au kukosa vipindi vyaa masomo darasani.
 - (h) Kutochemea shati na kuvalaa suruali bila mkanda kwa wavulana
 - (i) Kuvalaa viatu vyaa wazi hasa wakati wa masomo mfano ndala na yebo yebo.
 - (j) Kwenda au kukaribia kumbi za starehe, vilabu vyaa pombe na nyumba za kulala wageni (**guest houses**)

B. MWANAFUNZI ATAFUKUZWA SHULE KWA MAKOSA YAFUATAYO

1. Wizi (**Kuiba chochote**)
2. Ulevi na kutumia madawa ya kulevyta.
3. Kupata mimba/ujauzito.
4. Kupigana au kumpiga mwanafunzi mwenzako mwalimu au mtumishi yeyote.
5. Makosa ya jina mfano kuua kuiba n.k.
6. Kuoa au Kuolewa
7. Kusababisha Mimba ndani nan je ya shule.
8. Kuchochea na kufanya Mgomo, kuvuruga Amani na usalama wa watu.
9. Kukataa kwa Makusudi Adhabu.
10. Utoro wa kudumu.
11. Kudharau bendera ya Taifa.
12. Kukosa uzalendo kwa kudharau Bendera ya Taifa, Picha za Viongozi, Wimbo wa Taifa, Fedha za Taifa Nembo ya Taifa na alama zingine za kitaifa.
13. Kujiachisha shule mwenyewe
14. Kumiliki simu nyumbani na shulenii.

NB: Sheria hizi ndizo msingi wa maisha ya mwanafunzi kwa kipindi chote cha uanafunzi wake azisome kwa umakini mkubwa na kuzielewa.

NAKUTAKIA MAANDALIZI MEMA

.....

WILLIAM G. KANYONDO

MKUU WA SHULE

TAMKO LA MZAZI KUKUBALI KUMSOMESHA MWANAE

Mimi.....mzazi/Mlezi wa
Mwanafunzi.....aliyechaguliwa
kujiunga na shule ya Sekondari Mtua kidato cha kwanza Mwaka **2021**.

- (i) Nimekubali kumsomesha mwanangu katika shule hii.
- (ii) Nitatii sharia za Elimu, kanuni na Miongozo nilizofahamishwa na uongozi wa shule.
- (iii) Naukubali Mwanangu apewe adhabu stahiki na kwa mujibu wa taratibu za shule na serikali endapo atafanya kosa
- (iv) Nitahakikisha mwanafunzi haendi vilabuni, kumbi za cinema na muziki pamoja na kwenye vijiwe vya kamali na Bangi.
- (v) Nitampatia vifaa na mahitaji yote kwa wakati.
- (vi) Nitatoa taarifa endapo mwanangu atashindwa kuhudhuria shulenii.
- (vii) Nitashirikiana na walimu na Bodi ya shule katika kufuatilia maendeleo ya Mwanafunzi.
- (viii) Nitahudhuria vikao vyote vya wazazi kwa mujibu wa ratiba ya shule na vya Dharura.

Endapo sitatimiza wajibu wangu nichukuliwe hatua za kisheria

Jina kamili la MZAZI.....

Saini ya mzazi.....

Namba ya simu/Baruapepe

TAMKO LA MWANAFUNZI KUTII SHERIA, TARATIBU NA KANUNI ZA SHULE.

Mimi.....niliyechaguliwa kujiunga kidato cha kwanza Mtua sekondari nakubali kuwa nitatii sharia zote za shule na kufuata kikamilifu ratiba ya shule na sitashiriki migomo shulenii katika kipindi chote cha uanafunzi wangu. Nitakuwa Mzalendo kwa nchi yangu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Endapo sitatimiza tamko hili nichukuliwe hatua za kinidhamu.

Saini ya Mwanafunzi

Jina kamili la Mwanafunzi.....

President's Office Regional Administration and Local Government

Mtama district council

Mtua secondary school

P.O. Box 520

Lindi

Date.....

Ref.no.MSS/FI/2021/.....

THE MEDICAL OFFICER

.....
.....
.....

RE: REQUESTS FOR MEDICAL CHECK UP FOR.....

Please kindly refer to the heading above,

The named person in this form and a letter has been selected to join our school so as continuing with secondary school studies.

- 1. Blood**
- 2. Stool**
- 3. TB.....**
- 4. Syphilis.....**
- 5. Urine.....**
- 6. Eye test.....**
- 7. Ears.....**
- 8. Pregnancy.....**
- 9. Heart diseases.....**

- 10. Diabetus**

- 11. phychiantric disorder.....**

**I have examined Mr / Miss..... and
consider that he/she is fit/not fit to be admitted at your school.**

Name of the medical practitioner tittle.....

Signature.....

Date official stamp.....